# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA TATU

**06 APRILI, 2017**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 06 APRILI, 2017

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa za Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 4 la tarehe 27/01/2017
(ii) Toleo Na. 5 la tarehe 03/02/2017
(iii) Toleo Na. 6 la tarehe 10/02/2017
(iv) Toleo Na. 7 la tarehe 17/02/2017
(v) Toleo Na. 8 la tarehe 24/02/2017
(vi) Toleo Na. 9 la tarehe 03/03/2017
(vii) Toleo Na. 10 la tarehe 10/03/2017
(viii) Toleo Na. 11 la tarehe 17/03/2017
(ix) Toleo Na. 12 la tarehe 24/03/2017

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Maoni ya Kamati hiyo juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Tume ya Uratibu na Udhibiti UKIMWI) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU OFISI YA WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

## III. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**19. MHESHIMIWA JEROME DISMAS BWANAUSI (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali iliahidi kujenga madaraja ya Shaurimoyo, Nakalola na Miesi:-

Je, ni lini madaraja hayo yatajengwa.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**20. MHESHIMIWA SOPHIA HEBRON MWAKAGENDA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Wakulima wa Chai wa Wilaya ya Rungwe wanauza majani ya Chai kati ya shilingi 230/= hadi 240/= kwa kilo, wakati wakulima wa Njombe wanauza majani ya Chai kwa shilingi

500/= kwa kilo huku kukiwa na Bodi moja na ni nchi moja:-

Je, kwa nini wakulima wa Chai Wilaya ya Rungwe wanalazimishwa kuuza majani mabichi ya Chai kwa bei ndogo kuliko wakulima wa Chai wa Wilaya za Njombe na Lushoto.

**21. MHESHIMIWA JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Kampuni ya Chai ya Maruku imekuwa sugu kwa kutowalipa Wakulima wanaoiuzia Chai pamoja na kutowalipa Wafanyakazi wake yenyewe:-

Je, ni kwa nini Serikali haichukui hatua ya kuwasaidia Wakulima na Wafanyakazi hao ili kupata haki yao.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**22. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kumekuwepo na malalamiko makubwa kwa Wafanyabiashara wa Zanzibar wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam kuwa meli za Zanzibar zinapovuka Malindi

hulipishwa fedha nyingi na mizigo kupimwa kwa CBM tofauti na ilivyokuwa kabla; huku baadhi ya Wafanyabiashara wengine wanachajiwa kwa tani ambapo ni nafuu kutokana na hali halisi ya mizigo yenyewe:-

(a) Je, ni sawa kwa vyakula (local goods) kama vile Viazi Mbatata, Dagaa, Mahindi, Dawa zinazopelekwa Hospitalini, Vitunguu kuchajiwa kwa CBM; na Je, ni kweli kunasaidia wafanyabiashara au kuwakandamiza kiuchumi hasa ikizingatiwa kuwa bidhaa zenyewe ni vyakula;

(b) Je, nia ya Serikali ni kuwakwamua Wananchi kiuchumi au kuwakandamiza hasa ikizingatiwa kuwa baadhi yao ni Wafanyabiashara wadogo wadogo;

(c) Je, ni sababu gani za msingi kwa Bandari hiyo kuchukua fedha wakati huduma nyingine hawazipati kwa miaka yote.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**23. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (KALIUA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ni Hifadhi yenye hadhi ya kipekee hapa nchini, Afrika na

Duniani kwa ujumla; Hifadhi hii ina vivutio vya kipekee pamoja na kuwa na matumizi mseto (*multiple land use*) ambapo Wanyama na Mifugo inachungwa pamoja; kutokana na upekee huo Hifadhi hii imetambuliwa na kuwekwa kwenye maajabu saba ya Dunia chini ya Shirika la Uhifadhi la Dunia (UNESCO):-

Je, Serikali ina mpango gani endelevu wa kuhakikisha hadhi ya Hifadhi hii inabaki kwenye ubora wake kwa ajili ya vizazi vya leo na vijavyo na pia kwa uchumi wa Taifa letu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI MKUU:**

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **DKT. T. D. KASHILILAH** |
| **06 APRILI, 2017** | **KATIBU WA BUNGE** |